



## Lengo Kuu: Usafiri

Afya yako ni muhimu kwetu, ndiyo maana manufaa yako yanajumuisha usaidizi wa kusafiri kuhudhuria miadi ya huduma za afya na huduma zinazotolewa kupitia Oregon Health Authority (OHP). Iwapo huna mbinu ya usafiri kwenda kuhudhuria miadi ya huduma ya afya, mshirika wetu **Ride to Care** anaweza kukusaidia kusafiri.

### Njia tatu za kufika kwenye miadi

**Timu ya huduma kwa wateja ya Ride to Care itashirikiana nawe kupata chaguo linalofaa zaidi na la gharama nafuu zaidi ili kutosheleza mahitaji yako:**



#### Usafiri wa umma

Tunatoa pasi za usafiri za kila siku au mwezi. Tutajadili miadi yako na kuamua kama pasi ya siku au mwezi inakufaa zaidi ziara zako zilizoratibiwa.



#### Fidia

Tunalipa ada ya kila maili kwa umbali wa kwenda na kurudi kwenye ziara za afya. Unaweza kujibeba kwa gari yako mwenyewe, au mtu mwingine anaweza kukubeba. Chapisha fomu ya uthibitishaji wa miadi kwenye **ridetocare.com** na uwaombe wafanyakazi wa ofisi ya mtoa huduma wako kuweka saini. Fedha za fidia huwekwa kwenye kadi ya malipo ya mapema.



#### Usafiri wa gari

Tunaweza kuratibu safari za kibinafsi na za kushiriki na watu wengi. Kulingana na mahitaji yako ya matibabu, tunaweza kutuma gari dogo, gari la kiti cha magurudumu, gari la machela au ambulensi isiyo ya dharura.



Una haki ya kuomba kupewa usafiri wa siku iyo hiyo au siku inayofuata. Hata hivyo, ikiwa ombi lako ni la muda mfupi, na mahitaji ya usafiri ni mengi, tutayapa kipaumbele maombi ya dharura ya kiafya.

Ili upate maelezo zaidi, wasiliana na **Ride to Care** kwa kupiga simu kwa **855-321-4899** au **TTY 711**

**Wasiliana na Ride to Care kwa kupiga simu 855-321-4899 au TTY 711** ili uone huduma inayokufaa. Kila unapopiga simu, tutakuuliza maswali kukuhusu wewe na aina ya usafiri unaoomba. Ikiwezekana, tafadhali tupigie angalau siku mbili za kazi kabla ya miadi ya huduma ya afya ili kujadili na kuratibu usafiri wako. Unaweza kuratibu mapema kwa hadi siku 90.

**Ikiwa una maswali yoyote, ipigie simu Huduma kwa Wateja ya CareOregon kwa 800-224-4840.**

## Usafiri ni huduma inayotolewa na CareOregon, mpango wako wa afya wa Medicaid. Pata maelezo zaidi kutuhusu hapa.

Watu wanapozungumza kuhusu Medicaid katika eneo la Oregon, huenda utawasikia wakitaja majina au herufi nyingi tofauti. Hii ni kwa sababu kuna mashirika mengi yanayohusika katika kuhakikisha unapata huduma inayokufaa. Utaelewaje haya yote?

### Ichukulie Medicaid katika eneo la Oregon kama piramidi

**Oregon Health Authority (OHA)** inaendesha mpango wa Medicaid katika jimbo zima la Oregon, unaoitwa Oregon Health Plan (OHP).



**Health Share of Oregon (HSO)** ni shirika linaloitwa shirika la utunzaji lililoratibiwa (CCO). Health Share ya Oregon inafanya kazi chini ya OHA kuhudumia wanachama wa OHP katika eneo hili la kaunti tatu.



**CareOregon** ni mojawapo ya watoa huduma kadhaa wa bima katika eneo hili la kaunti tatu ambao husaidia Health Share CCO kutoa huduma. Huduma za usafiri hutolewa chini ya CareOregon.



**Mtoa huduma wako wa msingi (PCP)** anaweza kuwa daktari, muuguzi, msaidizi wa daktari au mtaalamu wa tiba asili. Ataratibu utunzaji wako na CareOregon na washiriki wengine wa timu ya matibabu kama vile madaktari wa meno, watoa huduma za afya ya akili, wanafamasia na wengine.



### CareOregon hutoa huduma kama hizi kwa wanachama wa Medicaid (OHP):

- ▶ Huduma ya afya ya kimwili
- ▶ Huduma ya afya ya akili
- ▶ Matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya
- ▶ Huduma ya meno
- ▶ Medicare kupitia CareOregon Advantage
- ▶ Huduma kwa wagonjwa mahututi kupitia watoa huduma za Housecall Providers

### Pia utaweza kutumia huduma muhimu kama hizi:

- ▶ Uratibu wa huduma
- ▶ Duka la dawa
- ▶ Utunzaji wa ujauzito na watoto wachanga
- ▶ Chaguo za usafiri
- ▶ Huduma za mkalimani wa lugha
- ▶ Huduma za dharura na haraka

### Una maswali?

Je, ungependa kujua zaidi? Ipigie simu timu yetu ya kirafiki ya **Huduma kwa Wateja kwa 800-224-4840** au ututumie ujumbe salama kupitia [careoregon.org/portal](https://careoregon.org/portal)

Unaweza kupata huduma hii kwa lugha nyinginezo, chapisho kubwa, Breli au kwa mfumo unaopendelea. Unaweza pia kuomba upewe huduma ya mkalimani. Usaidizi huu unatolewa bila malipo. Piga simu kwa 800-224-4840 au TTY 711.